# HALMASHAURI YA WILAYA YA RORYA

SHULE YA SEKONDARI NYATHOROGO,

S.L.P 230,

TARIME.

01/12/2023.

**Kumb.Na.NYASS/JI/46/14.**

**Ndugu**..............................................................................................

**YAH: <u>MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI NYATHOROGO ILIYOKO WILAYA YA RORYA MKOA WA MARA MWAKA-2024.</u>**

**1.0 UTANGULIZI**

Kwa niaba ya jumuia nzima ya Nyathorogo sekondari nachukua furusa hii kukupongeza na kukutaarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Nyathorogo kidato cha kwanza mwaka **2024**. Hongera sana na karibu sana.

Kumbuka nafasi hii uliyopata bado ni adimu miongoni mwa Watanzania walio wengi. Hivyo nakuomba kamwe usiichezee isije ikakuponyoka.

Muhula wa kwanza wa masomo unaanza tarehe **08/01/2024** mwisho wa kuripoti ni **19/01/2024** baada ya tarehe hiyo ya mwisho hautapokelewa na mzazi wako atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Ni marufuku kwa mwanafunzi kupanga. Mwanafunzi atakaye taka kupanga sharti awe na barua kutoka ofisi ya mkuu wa shule na ofisi ya mtendaji wa kijiji husika. Mzazi atakaye mpangishia mototo wake kiholela atachukuliwa hatua za kisheria.

**2.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA**

**2.1 Sare za shule (school uniform)**

- Wavulana-suruali mbili (nyeusi moja na damu ya mzee moja ) zenye malinda na zisiwe **modal** na shati mbili nyeupe mikono mifupi.
- Wasichana-Sketi mbili **-ndefu zinazogusa viatu** (nyeusi na damu ya mzee) zenye malinda inchi mbili kutoka rinda moja hadi lingine marinda madogo) na shati mbili nyeupe mikono mifupi.
- Viatu vya ngozi vyeusi vyenye kamba na visiwe na visigino virefu wala **muundo wa boot**. Hivi ni kwa wote (Wavulana na wasichana) na vinatakiwa pea mbili kwa kila mmoja.
- Soksi nyeupe kwa wavulana na wasichana.
- **Viatu** vya raba, bukta rangi ya njano na **T-shirt** rangi ya kijani yenye kora nyeusi kwaajili ya michezo.
- **Sweta** ya bluu (kwa wote) pamoja na **Tai** mbili (nyeusi na damu ya m zee)

**2.2 Vifaa vya darasani**

- Madaftari kumi na mbili (12) makubwa (quire 3)
- Karatasi za kutosha kwaajili ya kufanyia mazoezi mbalimbali (Rimu paper double A moja (01)
- Kalamu za wino nne (4)
- Kalamu za risasi (penseli 4)
- Mkebe wa hesabu (mathematical set-compasi -01)
- File binafsi la mwanafunzi (aje nalo siku ya kuripoti)

**3.0 SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.**

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya Elimu na.25 ya kwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozi yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi Teknolojia yenye dhamana ya Elimu Nchini na Ofisi ya Raisi –TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu. Hivyo unatakiwa kuzingatia na kufuata mambo yote ya msingi na sheria za shule kama zinavyooneshwa hapa chini.

Shule haitavumilia mwanafunzi mzembe anayetoa visingizio vya kutofanya kazi ndani na nje ya darasa. Mwanafunzi mwenye matatizo ya kiafya yajulikane tangu mwazo kupitia kwa daktari wa hospitali ya serikali. Hatutakubaliana na maelezo ya mdomo kuhusu matatizo ya kiafya ya mwanafunzi.

**3.1 MAMBO AMBAYO KILA MWANAFUNZI ANAPASWA KUFANYA.**

1. Kufuata taratibu zote kama zitakavyooneshwa katika ratiba ya shule na kama zitakavyokuwa zinatolewa na uongozi wa shule mara kwa mara.
2. Kuwa na utii na heshima kwa walimu, wazazi, walezi, wafanyakazi wa shule, viongozi na raia wote kwa ujumla.
3. Kuheshimu Bendera na Wimbo wa Taifa
4. Kulinda maadili ya **KAULI_MBIU** ya shule.
5. Kutumia lugha ya kiingereza daima na wakati wote unapokuwa shuleni.
6. Kushirikiana, kuthaminiana na kuheshimu kazi/maagizo yote yatolewayo na uongozi wa shule.

HEADMASTER,
NYATHOROGO SEC. SCHOOL
P.O.Box 230 TARIME

7. Kuzingatia usafi binafsi wa mwili na mazingira ya shule wakati wowote na kila mahali.
8. Kuhudhulia shuleni na vipindi vyote vya masomo ndani na nje ya darasa.
9. Kuzingatia ahadi.
10. .kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
11. . Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa.
12. . kutunza mali ya umma.

**3.2 MAMBO AMBAYO MWANAFUNZI HARUHUSIWI KUFANYA.**

1. Kuvuta sigara/bangi
2. kufuga kucha ndefu na nywele ndefu.
3. kufuga ndevu
4. kuvaa sare ya shule isiyo na heshima ya kubana na fupi.
5. kugombana.
6. kuiga mitindo ya kihuni, kama kunyoa kipara, kupaka kucha rangi n.k
7. kuchubua ngozi ya mwili kwa kutumia dawa n.k
8. Wageni wa wanafunzi hawaruhusiwi kuwasiliana nao pasipo kuwa na idhini ya uongozi wa shule wakati wa masomo.
9. Kwenda nje ya shule bila ruhusa wakati wa masomo.
10. Kuvaa kofia, bangili na mapambo mengine yoyote.
11. Kutohudhulia shule (masomo)

**3.3 MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE MARA MOJA NI;**

1. Wizi.
2. Uasherati, ubakaji na ushoga.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile bangi, cocaine, mirungi, kubeli n.k
4. Makosa ya jinai.
5. Kupigana au kupiga.
6. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
7. Kudharau Bendera au Wimbo wa Taifa.
8. Kuoa au kuolewa.
9. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani na nje ya shule.
10. Kutoa mimba.
11. Kugoma, kuchochea na kuongoza fujo zenye kuvuruga amani na usalama wa watu.
12. Kukataa adhabu makusudi.
13. Kuwa na simu ya mkononi.

**4.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA NA KUWASILISHA SHULENI NA MWANAFUNZI SIKU YA KURIPOTI.**

1. Medical examination form ( fomu inayoonyesha afya ya mwanafunzi) ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikari. Fomu hii itakabidhiwa kwa mkuu wa shule utakaporipoti shuleni.
2. Fomu ya maelekezo binafsi kuhusuhistoria ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai.
3. Fomu ya mzazi kukiri kukubariana na sheria kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule .
4. Cheti cha kuzaliwa cha mwanafunzi husika

**5.0** Tafadhari soma kwa makini maelezo/ maagizo na kuyatekeleza kikamilifu.

Mwisho nakutakia maandalizi mema na karibu sana Nyathorogo sekondari.

**GEORGE T.MINANAGO**
**MKUU WA SHULE.**

HEADMASTER, NYATHOROGO SEC. SCHOOL P.O.Box 230 TARIME.

**SIMU: MKUU WA SHULE-0684646938**
**MAKAMU MKUU WA SHULE-0756948112**

HEADMASTER,
NYATHOROGO SEC. SCHOOL
P.O.Box 230 TARIME.

**KIAMBATISHO C**

# NYATHOROGO SECONDARY SCHOOL

## FORM FOR MEDICAL EXAMINATION

FULL

NAME.........................................................................................................................

AGE............SEX.............HEIGHT........................WEIGHT...............................

Blood count (Red and White).................................................................................

Stool examination..................................................................................................

Urinalysis ...............................................................................................................

Eye test ..................................................................................................................

Ears ........................................................................................................................

Chest ......................................................................................................................

Abdomen ................................................................................................................

Plano test (girls) ....................................................................................................

Spleen ....................................................................................................................

I certify that the above named student is fit/unfit to pursue secondary education as stated above

Signature ...........................................................

Designatiuon ......................................................

Station ...............................................................

Date ..................................................................

KIAMBATANISHO 'D'

**FOMU YA MAELEZO YA BINAFSI YA MWANAFUNZI NA AHADI YA MWANAFUNZI NA MZAZI**

FOMU HII IJAZWE KIKAMILIFU KISHA MWANAFUNZI AILETE SHULENI SIKU YA KURIPOTI

**(i) MAELEZO BINAFSI YA MWANAFUNZI:**

1. Jina kamili la mwanafunzi.......................................................................................
2. Tarehe ya kuzaliwa ........................................................................................
3. Kabila ..................................................................................................
4. Dini ....................................................................................................
5. Shule aliyotoka .........................................................................................
6. Mwanafunzi anatoka Mkoa wa ...................wilaya ya .................Tarafa ya ..............Kata ..............................kijiji/Mtaa ...................Kitongoji .................
7. Jina kamili la Baba........................................................................
8. Jina kamili la mama .......................................................................
9. Anwani kamili ya baba/mlezi ...............................................................
10. Kazi anayofanya Baba/Mlezi .............................................................

**(ii) AHADI YA MWANAFUNZI**

Mimi ..........................................nakubali kwa dhati nafasi hii niliyopewa na Taifa kujiunga na shule ya sekondari Nyathorogo. Hivyo naahidi kwamba nitafata sheria, kanuni na taratibu zote za shule kama zilivyotolewa na kama zitavyoendelea kutolewa na uongozi wa shule

Sahihi ya mwanafunzi ..........................................

Jina la mwanafunzi ........................................................Tarehe .....................

**(iii) AHADI YA MZAZI/MLEZI** (Ijazwe na mlezi ikiwa tu baba na mama wa motto si hai)

Mimi ..........................................................ambaye ni Mzazi/Mlezi wa mwanafunzi nathibitisha kuwa taarifa zilizojazwa na mwanangu hapo juu ni za kweli na sahihi. Mimi nimezisoma sheria, kanuni na taratibu za shule ya sekondari Nyathorogo ambayo mwanangu amechaguliwa kujiunga, Hivyo naahidi kwamba;-

1. Nitamhimiza daima mwanangu kufuata kanuni, sheria na taratibu za shule
2. Nitashirikiana na uongozi wa shule katika malezi bora ya mwanangu ili kumuandaa kuwa raia bora wa Taifa letu
3. Nitampatia mwanangu mahitaji yake yote muhimu ya shule ili kumwezesha kuendelea na masomo hadi mwisho.

Sahihi ya Mlezi/Mzazi ..........................................

Jina la Mzazi/Mlezi .............................................

Tarehe ...........................................................

HEADMASTER,
NYATHOROGO SEC. SCHOOL
P.O.Box 230 TARIME

**Futa isiyotakiwa.**